

**KUBORESHA KWA KITUO CHA KILIMO CHA KIBAKWE (DODOMA)**

Mradi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (LIC) ni mradi wa kuendeleza sekta binafsi unaofadhiliwa na Danida. Mradi unashughulikia vikwazo vikuu vinavyokwamisha maendeleo ya biashara na ukuaji wa uchumi katika ngazi ya wilaya kwenye mikoa miwili ya Dodoma na Kigoma nchini Tanzania. LIC imejikita katika mijadala kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, miundombinu ya utoaji wa huduma za biashara ikiwa ni pamoja na vituo vya pamoja vya biashara na miundombinu ya pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kusaidia maendeleo ya biashara na uwekezaji. Washirika wanaotekeleza mradi wa LIC ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekretariati za mikoa ya Kigoma na Dodoma, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) Tanzania, Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

Kituo cha kilimo cha Kibakwe kiko chini ya wizara ya kilimo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwawa. Kituo kilianzishwa kwa ajili ya kutoa elimu ya kilimo – ya nadharia na vitendo kwa jamii ya kata ya Kibakwe. Mwezi wa kumi na mbili mwaka 2015, LIC ilipokea ombi kutoka halmashauri ya wilaya ya Mpwawa kusaidia kumaliza ujenzi wa mabweni ya wanafunzi (hosteli) na kuweka zana muhimu za elimu. Kwa kusaidia uwekezaji huu mradi wa LIC ulipendekeza kuanzishwa kwa muundo mpya wa usimamizi kwa njia ya (SPV) ambapo unajumuisha mkataba wa muendeshaji binafsi katika kusimamia shughuli za kituo.



Hosteli ya kituo cha kilimo cha Kibakwe kwa ajili ya kuhudumia wanafunzi (Upande wa mbele)



Hosteli ya kituo cha kilimo cha Kibakwe (Upande wa nyuma)

Mbali na kumaliza ujenzi wa hosteli, msaada wa LIC pia ulijumuisha uchimbaji wa kisima cha maji, ununuzi na ufungaji wa mfumo wa umwagiliaji wa dripu, uanzishwaji kwa kitalu kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu za mboga na miche iliyoboreshwa ya matunda, ununuzi wa vifaa vya ICT, ufungaji wa huduma za mtandao, ununuzi wa mashine muhimu za kilimo na zana kwa kituo hicho, na mwisho lakini sio kwa udogo, kusaidia maendeleo ya mipango mafunzo ya wakulima ikiwa ni pamoja na wakulima wadogo.



Bustani ya mbogamboga inayotumika kwa kujifunzia katika kituo cha kilimo cha Kibakwe



Tanki la maji lililo inuliwa maalum kwa kilimo cha umwagiliaji wa dripu

### **Mambo muhimu na mafanikio**

Kuboreshwa kwa miundombinu na programu za mafunzo kwenye kituo cha Kibakwe kimwezesha wilaya ya Mpwawa kutoa mafunzo bora kwa wakulima na vijana. Mfano mmoja ni vocha 30 za ujuzi kwa vijana, mradi unaendeshwa kwa ushirikiano na bodi ya mikopo na taasisi binafsi ya Kilimo na Mifugo (Visele) huko Mpwapwa, wamefanya mafunzo ya vitendo katika vituo. Pia wakulima wa mbogamboga saba walio karibu na kituo na maafisa ugani sita wamepata ujuzi wa kilimo cha mbogamboga kilichoboreshwa na kuwawezesha zaidi kuhudhuria mafunzo katika kituo cha mafunzo ya mbogamboga SEVIA mkoani Moshi.

Tangu kukamilika wa msaada wa LIC mwezi wa tatu mwaka 2018, kituo kimechukua jumla ya wakulima 170, pamoja na vijana 60 kufanya mafunzo ya kilimo cha maua na mbogamboga kwa miezi 6. Na awamu ijayo ya msaada wa mradi utaangalia njia za kusaidia vijana kuanza uzalishaji wa kibiashara wa bidhaa za mboga mboga pamoja na msaada kwa uwekezaji bora katika usindikaji.

Msaada wa LIC umeweka lengo la kituo kufikia kujitegemea kifedha kupitia mfumo wa usimamizi wa SPV. Mapato kutoka kwenye hosteli na warsha pamoja na mauzo ya mazao ya kilimo kwa kiasi kikubwa yatapunguza haja ya msaada wa kifedha kutoka kwenye halmashauri ya wilaya. Mradi huu umeonyesha kuwa kuna uwezekano wa kuanzisha vitu kama kituo cha mafunzo kupitia jitihada za ushirikiano baina ya mamlaka za wilaya na sekta binafsi. Hiki kituo kipekee kinalenga sekta ya ukulima wa maua na mbogamboga, lakini mfumo uliotumiwa hapa unaweza kutumiwa kwa minyororo mingine ya thamani katika mahitaji ya vifaa vya elimu na mafunzo ya gharama nafuu na fursa mbalimbali.

LIC imewekeza karibu shilingi milioni 194 kwa ajili ya kuboresha kituo cha kilimo cha Kibakwe.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya mradi: [www.lic.or.tz](http://www.lic.or.tz)